

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI



13/04/2018

Tenda Na. LGA- 045/2018-19/HQ/NC/01

TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi inakaribisha maombi ya Zabuni toka kwa Makampuni yenye sifa stahiki na uwezo kisheria kufanya kazi ya huduma ya uwakala wa ukusanyaji mapato kama inavyojionyesha katika jedwali hapa chini, katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, kwa kipindi cha kuanzia tarehe 01/07/2018 hadi tarehe 30/06/2019.

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI	IDADI YA "LOT"	ADA YA ZABUNI KWA KILA "LOT"
LGA/045/2018-2019/HQ/REV/01	Uwakala wa kukusanya Mapato ya masoko	LOT 1 - 16	50,000/=
LGA/045/2018-2019/HQ/REV/02	Uwakala wa kukusanya mapato vyoo vya Umma	LOT 1 - 6	50,000/=
LGA/045/2018-2019/HQ/REV/03	Uwakala wa kukusanya Ushuru wa Maegesho ya mabasi makubwa na madogo - STAND KUU	LOT 1	100,000/=
LGA/045/2018-2019/HQ/REV/04	Uwakala wa kukusanya Ushuru wa Maegesho ya magari na kudhibiti matumizi ya barabara (wrong parking)	LOT 1	100,000/=

LGA/045/2018-2019/HQ/REV/05	Uwakala wa kukusanya madeni Sugu ya Halmashauri	LOT 1	100,000/=
LGA/045/2018-2019/HQ/REV/06	Upangaji wa Maghala ya kuhifadhi Mizigo Soko la Kiusa	LOT 1	50,000

1. BARUA ZA MAOMBI ZIAMBATANISHWE NA MAELEZO KAMILI NA VIVULI (vilivyothibitishwa) vifuatavyo:-

1. Leseni (halali) ya Biashara husika.
2. Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni
3. Stakabadhi uliyolipia Ada ya Maombi ya Zabuni
4. Maelezo ya kazi ulizowahi kufanya na uzoefu usiopungua miaka miwili wa huduma ya Uwakala wa ukusanyaji Mapato na Vielelezo vilivyothibitishwa na Waajiri wa awali kwa kazi husika.
5. Usajili wa TIN
6. Usajili wa VAT (*Kama inahusika*).
7. Uthibitisho wa ulipaji Kodi (*Tax Clearance Certificate*) ya mwaka 2016/2017
8. Muombaji ataje kiasi (*Asilimia ya Commission atakayolipwa*) na Halmashauri kutokana na mchanganuo wake kati ya asilimia 1% -20%.
9. Muombaji aonyeshe idadi ya Wafanyakazi/Watendaji wake pamoja na sifa za Kitaalumu, Uzoefu/Ujuzi na Maadili ya kazi ya Huduma ya Ukusanyaji Mapato [uthibitisho unahitajika].
10. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonyesha *Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement)* ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyoidhinishwa na kuthibitishwa na *Meneja wa Tawi la Benki husika*.
11. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (*Power of Attorney*) wa mtu atakayehusika na Zabuni hii.
12. Muombaji aoneshe Taarifa za Hesabu za Kampuni za miaka miwili (2) hadi mitatu (3) iliyomalizika kabla ya kuomba Zabuni hii zilizokaguliwa na kuthibitishwa na Mkaguzi wa Hesabu (*aliyethibitishwa – Certified Public Accountant/Auditor*).

13. Taarifa ya madeni yake yote [kama yapo] anayodaiwa na watu binafsi, Benki au Taasisi nyingine.
14. Mzabuni anaweza kuomba zaidi ya Chanzo kimoja Kila aina ya zabuni italipiwa ada kama ilivyoonyeshwa katika jedwali.
- (i) Zabuni itakayowasilishwa bila kukamilika itaondolewa katika hatua za awali.
- (ii) Tathimini na tuzo itatolewa kwa Mzabuni kwa kuzingatia chanzo kimoja alichoshinda au mchanganyiko wa Vyanzo.
15. Mwisho wa kurudisha maombi ya zabuni ni tarehe **3/05/2018** saa **4.00** asubuhi siku ya Alhamisi ambayo ufunguzi utafanyika. Juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja aina ya Zabuni, Namba ya Zabuni na Lot. Zabuni hizo zipelekwe katika sanduku la Zabuni lililopo Ofisi **Na 35** kwa kutumia anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa, Manispaa ya Moshi, S.L.P. 318, MOSHI. Zabuni itakayochelewa haitafunguliwa. Kabrasha la Zabuni lina patikana Ofisi **Na 35** kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni. Mwombaji/Mwakilishi anaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni utakaofanyika tarehe 3/05/2018 saa 4.00 asubuhi, kwenye Ukumbi wa Mikutano Manispaa ya Moshi. kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu wa Bodi ya Zabuni, chumba na 35 moshi manispaa.

Michael N. Mwandezi
MKURUGENZI MANISPAA
MOSHI